*Kioo cha Lugha, Juz. 19(2), 2021, 92-102*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.*

# Ufaafu wa Matumizi ya Nadharia ya Utabia katika Mbinu za Kufundishia Lugha ya Kigeni

*Saul Bichwa*[1] *na Faraja Mwendamseke*

## Ikisiri

Makala hii inadhamiria kuchunguza kwa undani Nadharia ya Utabia ambayo ni miongoni mwa nadharia zinazotumiwa katika kufundisha lugha ya kigeni. Uchunguzi huu unazingatia mtazamo wa B. F. Skinner, mwanasaikolojia maarufu wa utabia na majaribio yake kwa wanyama. Hivyo, dhana ya tabia imeelezwa bila kuhusisha matukio ya kiakili na michakato ya ndani kwenye ubongo, bali inahusishwa na sababu za nje za kimazingira. Nadharia ya Utabia, kama ilivyo leo, inazidi kuachwa nyuma taratibu kutokana na kuwapo kwa nadharia nyingi za ufundishaji lugha. Hii inatokana na tafiti jaribizi kuonesha upungufu katika Nadharia ya Utabia (VanPatten na Williams, 2015). Hata hivyo, ipo haja ya kuonesha kwamba kiuhalisia, Nadharia ya Utabia bado ina umuhimu katika shughuli fulani za ufundishaji na ujifunzaji darasani. Data za utafiti huu zimekusanywa uwandani kwa kutumia mbinu ya mahojiano na hojaji. Matokeo ya utafiti yamebaini kuwa mbinu zinazotokana na nadharia hii zina umuhimu katika ujifunzaji darasani kwa sababu zinazingatia tabia lengwa, ushiriki wa wajifunzaji na tokeo. Hii ina maana kuwa ni lazima mjifunzaji afanye mazoezi ya kusikiliza/kuzungumza au kuandika/kusoma kwani bila kufanya hivyo, tokeo la kuwasiliana halitaonekana. Hata hivyo, haya yote yatategemea malengo ya mjifunzaji na muktadha wa ufundishaji. Hii inadhihirisha kuwa tabia ya ujifunzaji inaonesha kuwa kuna mwingiliano mkubwa kati ya mwitikio wa kitabia na kichocheo husika.

## 1.0 Utangulizi

Kwa mujibu wa Skinner (1976), ujifunzaji ni mchakato wa marekebisho ya kukabiliana na hali, kupitia uigaji na marekebisho kati ya vitengo muhimu vya

[1] Mhadhiri, Idara ya Lugha na Fasihi, Kitivo cha Humanitia na Sayansi za Jamii, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: mwalimubichwa@gmail.com, bichwa.saul@duce.ac.tz

Mwendamseke ni Mhadhiri, Idara ya Lugha na Fasihi, Kitivo cha Humanitia na Sayansi za Jamii, Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Tanzania. Baruapepe: fmwendamseke@gmail.com

kuhamasisha utambuzi wa mtu fulani. Katika mtazamo wa saikolojia, tabia inakosa ishara kwenye mwingiliano kati ya kichocheo na mwitikio. Mtu huchukuliwa kuwa amejifunza kitu kama anaweza kuonesha mabadiliko katika tabia. Kwa mujibu wa nadharia hii, umuhimu wa ujifunzaji hutegemea muundo/aina ya ingizo, kichocheo na matokeo kwa muundo wa mwitikio. Kwa muda mrefu kumekuwa kukitafutwa njia bora inayoweza kutumiwa kufundisha lugha ya kigeni kwa ufasaha. Miongoni mwa nadharia zilizoundwa ili kueleza njia iliyo bora ya kufundisha lugha ya kigeni kwa ufasaha ni Nadharia ya Utabia. Nadharia hii iliasisiwa na Ivan Petrovich Pavlov, John Broadus Watson, Edward Lee Thorndike na Burrhus Frederic Skinner. Hii ni miongoni mwa nadharia za awali zinazohusu ujifunzaji lugha za kigeni zilizoundwa kabla ya miaka ya 1990, iliyotokana na taaluma ya saikolojia (VanPatten na Williams, 2015).

VanPatten na Williams (2015) wanaeleza kuwa Nadharia ya Utabia inayo mihimili mitatu. Mihimili hiyo ni uzoeshi, uimarisho chanya, na uimarisho hasi. Nadharia ya Utabia inaona kuwa ujifunzaji na mabadiliko ya tabia ya wanafunzi hutokana na kuzalisha matokeo kwa kuzungumza au kuandika, nalo jukumu la mwalimu ni kudhibiti kichocheo na mazingira ya ujifunzaji ili kubadilisha hatima inayotarajiwa. Uimarisho chanya wa ingizo sahihi na kukosoa kisicho sahihi huwezesha mchakato wa ujifunzaji kufanikiwa.

Mtazamo wa wanautabia kuhusu ujifunzaji huangalia jinsi tabia ya wajifunzaji inavyojengwa kupitia kichocheo na mwitikio. Pia, huchukulia kwamba tabia hudhihirika kwa kuonekana katika mazingira husika. Nadharia hii ina mfumo wa dhana na kanuni, hivyo, nadharia hii ni muhimu kwani humsaidia mwalimu kutambua tukio katika ulimwengu wa kujifunza (Lodico na wenzake, 2006).

Licha ya kwamba manufaa ya Nadharia ya Utabia yanaweza kuonekana katika ujifunzaji wa darasani wa kila siku, kuna wataalamu kama vile Gadza na Raymond (1980), Brown (1994) na Fauziati (2014) wanadai kuwa nadharia hii haifai kutumiwa katika kufundishia lugha ya kigeni. Mojawapo ya sababu zinazotolewa za kutofaa kwa nadharia hii ni: si wakati wote wajifunzaji hujifunza kwa kurudia bali huweza kujiundia miundo ya lugha wenyewe na kurekebishwa. Ndipo nadharia nyingine zilipoibuka kujaribu kuelezea namna ya kufundisha lugha za kigeni. Hali hii, ilisababisha nadharia za awali ikiwamo ya Utabia kufifia kutokana na udhaifu uliojitokeza.

Maelezo haya yanaonesha kuwa kuna umuhimu wa kuendeleza mjadala kuhusu Nadharia ya Utabia. Kwa sababu hiyo, makala hii imeeleza kwa ufupi mtazamo wa jumla wa Nadharia ya Utabia, jinsi nadharia hii inavyotumika katika mbinu za ufundishaji wa lugha za kigeni na ufaafu wake katika mchakato wa ufundishaji lugha ya kigeni leo. Tunatumaini kuwa mjadala huu utasaidia kujenga hoja kwamba Nadharia ya Utabia ina mchango chanya katika ufundishaji wa lugha ya kigeni, hatimaye, kuleta uelewa wa kwa nini walimu wanachagua mbinu fulani

kuwafundisha wanafunzi fulani wenye malengo fulani ya ujifunzaji. Makala hii imegawanyika katika sehemu nne. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili ni ufafanuzi wa Nadharia ya Utabia pamoja na mikabala inayofungamana nayo. Sehemu ya tatu inafafanua jinsi Nadharia ya Utabia inavyofaa katika ufundishaji wa lugha ya kigeni, na sehemu ya nne ni hitimisho.

## 2.0 Nadharia ya Utabia

Nadharia hii ya ujifunzaji ilikitwa katika matokeo yanayoweza kupimwa, kuonekana, kuchambuliwa na kuthibitishwa kwa usahihi. Hivyo, marudio katika ujifunzaji yalitumika ili kuifanya tabia iliyokusudiwa kuwa desturi. Matokeo yaliyotarajiwa katika matumizi ya Nadharia ya Utabia ni kuundwa kwa tabia iliyokusudiwa. Tabia iliyokusudiwa hupata uimarisho chanya, nayo tabia isiyofaa hutunukiwa uimarisho hasi. Tathmini hufanywa kwa kuangalia tabia zinazoonekana. Katika nadharia hii, walimu wengi hawatoi maelezo mengi, bali hutoa maelekezo machache yanayofuatiwa na mfano ama kutoka kwa walimu wenyewe au kupitia kichocheo fulani (Skinner, 1976).

Nadharia ya Utabia na kielelezo chake cha uhusiano kati ya kichocheo na mwitikio humchukulia mtu kama mjifunzaji anayejitegemea (Alissa, 2003). Miitikio maalumu ya tabia huchambuliwa kwa kutumia mbinu za ufundishaji au mazoea pekee. Kujitokeza kwa tabia huimarika zaidi pindi uimarisho chanya unapotolewa, na hutoweka pindi adhabu inapotolewa. Mtu huchukuliwa kuwa amejifunza kitu fulani kama ataweza kuonesha mabadiliko ya tabia. Kwa mujibu wa nadharia hii, ujifunzaji muhimu upo katika mfumo wa ingizo, kichocheo na matokeo kwa mfumo wa mwitikio wa kichocheo hicho.

Kichocheo ni kile ambacho mwalimu humpa mwanafunzi na mwitikio ni aina ya athari au jibu la mwanafunzi kutokana na kichocheo hicho kilichotolewa na mwalimu. Mchakato unaotokea kati ya kichocheo na mwitikio hauwezi kuonekana na hauwezi kupimwa (Sarah, 2006). Kinachoweza kuonekana ni kichocheo na mwitikio.

Hivyo basi, kile kinachotolewa na mwalimu (kichocheo) na kile kinachokubaliwa na wanafunzi (mwitikio) ndicho kinachotakiwa kionekane na kipimwe (Fauziati, 2016). Hii inadhihirisha kwamba upimaji ni kitu muhimu katika kugundua iwapo mabadiliko ya tabia yametokea au la. Aidha, Nadharia ya Utabia inahusisha Nadhariatete ya Uzoeshi ya Pavlov, Masharti ya Watson, Ushikamani ya Thorndike na Uzoeshi-fanyizi ya Skinner, ambazo tunazifafanua katika sehemu inayofuata.

### 2.1 Nadhariatete ya Uzoeshi ya Pavlov

Nadhariatete hii imeegemea katika madai ya Pavlov kwamba kichocheo-asili kinapowekwa pamoja na kichocheo-masharti kisicho bainifu kwa kurudiarudia, hujenga tabia fulani. Majaribio yaliyofanywa na Pavlov na wataalamu wengine

yanaonekana kuathiriwa sana na mitazamo ya Nadharia ya Utabia ambayo ni mitazamo ya kisaikolojia kuhusu tabia ya mtu.

Kuielewa Nadhariatete ya Uzoeshi kwa jumla, kunahitaji kuelewa kuwa kuna aina mbili za vichocheo na aina mbili za miitikio. Aina hizo mbili ni kichocheo huria, ambacho moja kwa moja huzalisha kichocheo kinachotangulia mwitikio/majibu pasi ujifunzaji wowote (kwa mfano, chakula); na kichocheo masharti, ambapo kichocheo kisicho bainifu huleta mwitikio-sharti baada ya kukihusianisha na kichocheo si-masharti (kwa mfano, chakula kinakuja kabla ya milio ya kengele).

Dhana kwamba kutumia vichocheo fulani kunaweza kubadilisha tabia ya binadamu inayokusudiwa, ilimfanya Pavlov kufanya majaribio akitumia mnyama (mbwa) kwa kuchukulia kuwa tabia za wanyama hufanana na za binadamu. Hata hivyo, pamoja na umuhimu wa jaribio hilo, kimsingi kuna tofauti baina ya binadamu na wanyama. Pavlov alikuwa anafanya majaribio kuhusu jinsi ya kufanyia upasuaji shavu la mbwa. Kufuatia upasuaji huo, tezi la mate linaonekana katika upande wa nje. Mbwa anapooneshwa chakula, tezi linatoka nje na mbwa anatoa mate. Sasa, kabla chakula hakijaoneshwa, mwanga mwekundu unaoneshwa kwanza, na baadaye chakula. Kwa kufanya hivyo, mate yatatoka yenyewe nje. Kama kitendo hicho kitafanywa kwa kurudiwarudiwa, kisha wakati mwingine, kwa kuonesha tu mwanga mwekundu bila chakula, mate yatatoka nje. Chakula ni kichocheo muhimu, wakati mwanga mwekundu ni kichocheo bandia. Kitendo hicho kikifanywa kwa kurudiwarudiwa, kitaleta uchochezi-masharti bandia utakaofanya mbwa kutoa mate. Tukio hili linaitwa uzoeshi au mwitikio wa tendohisia lililozoeshwa.

## 2.2 Nadhariatete ya Masharti ya Watson

Watson ni mwananadharia ya utabia halisi. Ametafiti kuhusu ujifunzaji na sayansi nyingine kama fizikia au biolojia ambazo zinahusu zaidi majaribio yanayothibitika pekee, yaani yanaweza kuonekana na kupimika. Kwa mujibu wa Watson, ujifunzaji ni mchakato wa mwingiliano kati ya kichocheo na mwitikio (Johnson, 2001). Kwa jambo hilo, kichocheo na mwitikio huimarishwa na tabia zinazoweza kuonekana na kupimika. Watson anakiri kuwapo kwa mabadiliko ya kiakili kwa mtu katika mchakato mzima wa ujifunzaji, na analiona jambo hilo kama lisilotakiwa kutiliwa maanani. Inaaminika kwamba katika mchakato wa masharti, tunaweza kujenga kundi la miunganiko ya kichocheo-miitikio, na tabia changamano zaidi zinafunzwa kwa kuunda mfuatano wa miitikio (Watson, 1913).

## 2.3 Nadhariatete ya Ushikamani ya Thorndike

Mtazamo wa Thorndike (1911) juu ya ujifunzaji ni kwamba ujifunzaji ni mchakato wa kuunda uhusiano au ushikamano au aliiita “muungano wa matendo fulani na hali fulani na matokeo mazuri”. Katika kudhihirisha muungano wa matendo, alisisitiza uzingatiaji wa sheria katika kujenga mahusiano yenye kuleta athari chanya katika kujifunza. Hivyo, Thorndike anazigawanya sheria za ujifunzaji kama ifuatavyo:

### 2.3.1 Sheria ya Utayari

Sheria hii inaeleza kuwa kiumbe atajifunza endapo tu atakuwa tayari kujifunza. Kiumbe anapokuwa tayari kupata mabadiliko ya tabia, kutimilizika kwa tabia hizo kutasababisha kiumbe huyo kuridhika na ndipo uhusiano unapoimarishwa.

### 2.3.2 Sheria ya Mazoezi

Inapendekeza kuwa kusoma kwa undani na kufanya mazoezi kunaongeza ufanisi na kudumu kwa ujifunzaji. Kanuni ya mazoezi ni muunganiko kati ya sharti (ambalo ni kichocheo) na mwitiko (tendo); ambapo tendo litakuwa imara zaidi kwa sababu ya mazoezi, ila tendo hilo litadhoofishwa kama muunganiko kati ya viwili hivyo haukuendelezwa. Hivyo, kanuni ya sheria hii inaonesha kwamba kanuni kuu ya ujifunzaji ni marudio. Kadiri ujifunzaji unavyorudiwa mara kwa mara, ndivyo somo hilo linavyoimarishwa zaidi.

### 2.3.3 Sheria ya Athari

Uhusiano huimarishwa kama kichocheo kinaleta matokeo mazuri na hudhoofishwa kama matokeo hayaridhishi. Sheria hii inaashiria miunganiko kuwa imara au dhaifu kutokana na matendo. Tendo linaloendeleza furaha litarudiwa tena kwa mara nyingine. Kinyume na hapo, tendo linaloleta matokeo yasiyofurahisha linasitishwa na halitarudiwa.

## 2.4 Nadhariatete ya Uzoeshi-fanyizi ya Skinner

Dhana zilizoelezwa na Skinner kuhusu ujifunzaji zinaweza kuzizidi ubora dhana nyingine zilizoelezwa na wataalamu wa awali. Skinner aliweza kuzielezea dhana kwa namna rahisi ya kujifunza. Kwa mujibu wa Skinner (1992), uhusiano kati ya kichocheo na mwitikio hutokea kupitia mwingiliano wa mazingira, ambao baadaye huleta mabadiliko katika tabia. Si rahisi kama ilivyoelezwa na wataalamu wa awali. Hivyo, ili kuielewa tabia ya mtu, ni lazima kwanza kuelewa uhusiano kati ya kichocheo kwa kila tabia, na kuelewa kuwa mwitikio unaweza kusababishwa na matokeo yanayoweza kutokea kutokana na mwitikio. Skinner pia ameeleza kuwa kutumia mabadiliko ya kiakili kama chombo cha kuielezea tabia huongeza ugumu wa tatizo.

Kati ya wadau wote wa Nadharia ya Utabia, nadharia ya Skinner ina ushawishi mkubwa zaidi. Programu za ujifunzaji, kama vile zana za kufundishia, moduli, na programu nyingine za ujifunzaji, zimekitwa katika dhana ya uhusiano wa kichocheo na mwitikio, mambo muhimu ya uimarishaji, na programu za ufundishaji zinazotekeleza nadharia ya ujifunzaji iliyopendekezwa na Skinner.

Kwa mujibu wa Skinner, ili kuimarisha tabia, tunahitaji uimarisho. Kuna aina mbili za uimarisho – uimarisho chanya na uimarisho hasi. Uimarisho chanya hukitwa katika kanuni kwamba idadi au kiwango cha mwitikio huongezeka kwa sababu hufuatiwa na kichocheo ambacho kina zawadi. Hivyo, tabia hutarajiwa kuongezeka kwa sababu hufuatiwa na kichocheo kinachofurahisha. Kwa mfano, wanafunzi

husoma kwa juhudi ili kushika nafasi nzuri na kushinda baiskeli watakayozawadiwa na wazazi wao. Ili tabia irudiwe au iboreshwe, kunahitajika kusoma kwa bidii ili kushika nafasi ya kwanza, na uimarisho chanya ni kuzawadiwa baiskeli.

Uimarisho hasi hutawaliwa na kanuni inayoelekeza kwamba kiwango cha miitikio huongezeka kwa sababu ya kufuatiwa na kichocheo kisichofurahisha. Hivyo, tabia inatarajiwa kuongezeka kwa kuondolewa kwa kichocheo kisichofurahisha. Kwa mfano, mwanafunzi anasema: "Nataka maji"; mwalimu anamkosoa kwa utaratibu: "Kutokana na tamaduni zetu Tanzania, tunasema: "Naomba maji". Kwa hiyo, ili tabia iweze kurudiwa/kusisitizwa, ni lazima kichocheo kisichofurahisha kiondolewe.

## 3.0 Nadharia ya Utabia katika Mbinu za Kufundishia Lugha za Kigeni

Nadharia hii ni muhimu katika kujifunza lugha za kigeni. Athari ya nadharia hii huonekana katika kutekeleza mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia mbinu ya kutafsiri sarufi, mbinu ya moja kwa moja, mbinu ya kufundisha lugha kihali inayohusiana zaidi na njia ya kufundishia lugha husika iitwayo mbinu ya kusikia na kusimulia. Hata hivyo, mbinu ya tafsiri haijapewa kipaumbele katika makala hii kwa sababu mwalimu anafunza kwa kutafsiri kutoka lugha inayofunzwa kwenda katika lugha ya kufundishia. Vilevile, mbinu ya moja kwa moja haijashughulikiwa kwa sababu hufunza kwa kuzingatia misingi ya lugha lengwa kwa kuwa kutambua lugha ni kuzungumza zaidi kuliko kuiandika. Kwa hiyo, yapo maarifa ya mbinu kuhusiana na kuzungumza yanapatikana katika mbinu ya kusikia na kusimulia. Hivyo, tumeteua mbinu hii kwa sababu moja kwa moja inahusisha ingizo na tokeo katika ujifunzaji lugha, jambo ambalo lina umuhimu wake.

### 3.1 Mbinu ya Kusikia na Kusimulia

Mbinu hii ya kusikia na kusimulia ina kanuni mbili: (i) dhana ya kichocheo-mwitikio, na (ii) wazo kwamba ujifunzaji lugha ya pili hutakiwa uakisi au ufuate michakato ya kujifunza lugha mama. Kwa mujibu wa Nadharia ya Utabia, mjifunzaji wa lugha ya kigeni huwa tayari na misingi ya lugha ya kwanza inayomsaidia kuhawilishia maarifa ya lugha mama kwenye lugha ya kigeni. Kama kuna ufanano kati ya lugha mama na lugha ya kigeni, uhawilishaji unaweza kumsaidia kujifunza lugha ya kigeni, au kumpotosha, kama lugha hizo hazifanani.

Kwa mujibu wa Fauziati (2016), sifa za Nadharia ya Utabia katika mbinu ya kusikiliza na kusimulia ni kama zifuatazo: (i) kiumbe ni mjifunzaji, (ii) tabia ni tabia ya maneno, (iii) kichocheo ni kile kinachotolewa katika lugha ya kigeni, (iv) mwitikio ni athari inayotolewa na mjifunzaji kutokana na kichocheo, na (v) uimarisho kama kibali na sifa kutoka kwa mwalimu, wanafunzi wenzake, na kuridhia kwa mtu binafsi katika kutumia lugha husika.

Kwa kuzingatia uhusiano kati ya Nadharia ya Utabia na mbinu ya kusikiliza na kusimulia, sasa ni wazi kwamba mbinu ya kusikiliza na kusimulia inasisitiza kuwa lugha mpya hutakiwa ifundishwe kwa kuzingatia mfuatano wa kusikiliza, kuzungumza, kusoma, na kuandika na msisitizo uwekwe katika kufundisha ujuzi wa

kupokea kabla ya ujuzi wa kuzalisha, kama inavyodaiwa na Alexander (1986) kama ilivyorejelewa na Johnson (2001). Johnson (2001) anadai kuwa hakuna kinachoweza kuzungumzwa kabla hakijasikilizwa, na hakuna kinachoweza kuandikwa kabla hakijasomwa. Sifa nyingine ni pamoja na kuunda mazoea kwa kurudiarudia mara kwa mara, kuzuia makosa, kuiga bila kutumia sauti, kukumbuka, na mbinu ya kuchunguza mambo kwa undani zaidi. Vilevile, mbinu ya kusikiliza na kusimulia inasisitiza kuzuia matumizi ya lugha mama darasani, badala yake itumike lugha lengwa sambamba na matumizi ya maabara ya lugha katika ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa mfano, kuhusiana na mbinu ya kuchunguza mambo kwa undani katika Nadharia ya Utabia, Brooks (1968), kama alivyorejelewa na Fauziati (2014), ametaja aina tofautitofauti za mazoezi yanayowezesha kuchunguza mambo kwa undani. Mazoezi hayo ni:

a) Marudio: kurudia usemi/maneno kwa sauti mara baada ya kuyasikia;
b) Uambishaji: kuweka viambishi katika mzizi wa neno;
c) Kubadili nafasi: kuweka neno mbadala katika usemi;
d) Umaliziaji: kuurudia usemi mzima;
e) Upanuzi: kuongeza neno katika sehemu fulani ya usemi;
f) Ufupisho: kubadili kishazi au kirai kwa neno moja;
g) Ubadilishaji: kubadili sentensi kuwa katika hali ya uyakinifu kwa kubadilisha njeo, hali, dhamira au kauli;
h) Uambatanishaji: Kuambatanisha semi mbili;
i) Kubainisha iwapo tungo ni ya kweli au si ya kweli; kutoa majibu/mwitikio sahihi kwa usemi uliotolewa;
j) Kupangilia maneno katika tungo; kuwataka wanafunzi warudishe mfuatano wa maneno kwenye sentensi kama ulivyokuwa kwenye sentensi asilia.

Kutokana na mchakato wa mbinu hii namna unavyotumika kufundishia lugha ya kigeni, ni hahiri kabisa kuwa mazoezi ya namna tofautitofauti yanapotumika katika darasa la kigeni huwajengea uwezo wa kuitumia lugha husika. Hii hutokana na kupata ingizo la kutosha na hatimaye kuweza kuonesha tokeo bora kwa sababu ya urudiajirudiaji wa mazoezi hayo. Aidha, mazoezi hayo yamepewa msisitizo kuanzia kwenye kusikiliza halafu ndiyo aweze kuzungumza, kuandika na kusoma. Kwa hiyo, mwalimu wa lugha ya kigeni hana budi kuzingatia hili katika ufundishaji wa lugha ya kigeni kwa sababu misingi hiyo ni faafu katika kujifunza lugha ya kigeni.

### 3.2 Mbinu ya Kufundisha Stadi ya Kuandika

Kama ilivyoelezwa bayana hapo awali, kwamba mazoezi ya darasani katika Nadharia ya Utabia yametawaliwa na sifa ya mwigo na kuzuia makosa. Kwa hiyo, Nadharia ya Utabia ina uhusiano wa karibu na mbinu ya kufundisha kuandika inayoitwa mbinu ya zao (Staats na Staats, 1963; Staddon, 2014). Mwigo wenyewe ni kuiga tabia au kauli. Katika kufundisha kuandika kama zao, hatua kuu zinahusisha mwigo na kubadilisha mifano inayotolewa na mwalimu, na kusisitiza kuzalisha zao

la mwisho lisilo na makosa. Katika mbinu ya zao, kazi za darasani huhusu zao la mwisho la kuandika na jinsi zao hilo linavyotakiwa lionekane kama mfano uliotolewa (Fauziati, 2014).

Aidha, katika mbinu hii mwalimu hana budi kutumia mifano ya kutosha. Pia, kuwe na mazoezi ya kurudiarudia kuandika. Kwa hiyo, tunaweza kusema kwamba Nadharia ya Utabia imekuwa faafu katika kufundisha kuandika kwa sababu inaweza kumjengea mjifunzaji uwezo wa kuandika kutokana na kupewa mifano sahihi na mazoezi ya kurudiarudia kuandika msamiati au tungo husika. Hivyo, humsaidia katika kujifunza lugha ya kigeni.

**4.0 Vielelezo katika Mchakato wa Ujifunzaji Lugha**

Kwa kuzingatia mbinu za ufundishaji lugha ya kigeni, Nadharia ya Utabia inatoa vielelezo vingi katika mchakato wa ujifunzaji wa lugha. Navyo ni vifuatavyo:

**i) Uundaji**

Kwa kawaida, walimu hufundisha mambo mepesi kwanza kabla ya kufundisha mambo magumu. Mambo magumu huweza kufundishwa kupitia uundaji au makadirio fanikiwa. Uundaji unaashiria njia zinazoimarisha makadirio mfululizo katika tabia muhimu. Mchakato huu unaanza na malengo ya utafiti, uchambuzi wa kazi, kazi za wanafunzi na mwitikio wao kwa motisha (Blankship, 1981). Blankship anataja hatua nne za tabia ya wanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji:

a) Kuja darasani kwa muda mwafaka;
b) Kushiriki vizuri katika mchakato wa ujifunzaji;
c) Kuonesha matokeo mazuri katika majaribio; na
d) Kufanya kazi zao za nyumbani.

**ii) Kuwa wa Mfano**

Kuwa wa mfano ni aina mojawapo ya ujifunzaji katika Nadharia ya Utabia. Mara nyingi, mwalimu wa lugha hutumia njia hii katika kufundisha lugha. Mwanafunzi huiga tabia ya mwalimu katika mchakato wa ujifunzaji. Kwa mfano, mwalimu wa Kiingereza anasoma kitabu cha Kiingereza mara kwa mara darasani katika mchakato wa kujifunza lugha. Hivyo, mwalimu ni mfano wa kuigwa kwa wanafunzi; kisha wanafunzi wataiga tabia hiyo. Wanafunzi pia watasoma mara kwa mara darasani kama mwalimu wao.

**iii) Kutuza na Kuadhibu**

Katika mchakato wa ujifunzaji, mara nyingi wanafunzi hutuzwa wanapopata matokeo mazuri katika ujifunzaji. Hata hivyo, mwalimu hutoa adhabu kwa wanafunzi wake kwa sababu ya makosa ya wanafunzi hao. Adhabu hii inatakiwa itolewe kwa namna ya busara darasani. Njia hii imekitwa katika nadharia ya Skinner ya kutuza na kuadhibu. Katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji, mara nyingi wanafunzi wanapata ugumu katika somo la lugha ya kigeni, hivyo, mara nyingi

hupata adhabu kutoka kwa walimu wao. Tuzo na adhabu ni moja ya viashiria vya Nadharia ya Utabia ya Skinner katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji hasa katika ujifunzaji lugha. Tuzo inapotolewa ili kuimarisha maendeleo ya ujifunzaji, husadifu uimarisho chanya ilhali kitu kisicho sahihi kinapokosolewa ili kuwezesha mchakato wa ujifunzaji kufanikiwa husadifu uimarisho hasi.

**iv) Ujifunzaji Pangilifu**

Ujifunzaji pangilifu ni aina mojawapo ya matumizi ya kanuni ya uzoeshi-fanyizi. Mchakato huu wa ujifunzaji hutokea pale wanafunzi wanapopewa kazi ya kufanya na mwalimu na kuifanya. Katika mchakato wa ujifunzaji lugha, mwalimu huwapa wanafunzi kazi ya kufanya, kusoma hadithi kwenye vitabu vyao vya lugha ya kigeni, na huifanya. Ujifunzaji pangilifu una malengo manne, nayo ni:

a) Kufanya muhtasari wa nyenzo za ujifunzaji;
b) Kuwalazimisha wanafunzi kusoma nyenzo za ujifunzaji;
c) Kutoa matokeo ya ujifunzaji moja kwa moja kwa mwalimu; na
d) Kutumia muda mwafaka katika ujifunzaji.

**v) Kutoa Kazi/Mazoezi ya Kufanya**

Kuna sehemu nyingi za kazi za ujifunzaji katika nadharia ya utabia, nazo ni:

a) Malengo na utafiti katika tabia;
b) Kugawanya kazi katika kazi ndogondogo;
c) Kutambua uhusiano kati ya kazi ndogondogo;
d) Kutambua nyenzo na hatua za kazi ndogondogo; na
e) Kutoa mrejesho mwishoni mwa kazi ndogondogo.

Vipengele hivi vya ujifunzaji vinamaanisha kuwa, kwa kawaida, wanafunzi hufanya kazi na kuzigawa katika kazi ndogondogo. Katika mchakato wa ujifunzaji lugha, kwa kawaida, wanafunzi hufanya mazoezi/kazi kutoka kwa mwalimu wa lugha, kisha matokeo huchambuliwa na mwalimu.

Kiashiria cha mwisho cha utabia katika kujifunza lugha kinahusiana na nadharia za uamiliaji lugha. Wanautabia wamegundua kuwa nadharia za uamiliaji lugha zimekuwa zikitumika hadi leo. Wanautabia wanaeleza kwamba mwanadamu huzaliwa akiwa haijui lugha, kwa maana ya kuwa *tabula rasa*, na wanadamu hujifunza lugha kutoka kwenye mazingira yao. Kwa hiyo, nadharia hii inatambua nafasi ya mazingira katika ujifunzaji lugha za kigeni. Hapa izingatiwe kuwa mazingira hutumika kwa maana pana zaidi, kwa kuhusisha masuala ya utamaduni wa jamii inayotumia lugha hiyo. Ujifunzaji lugha ni sawa na ujifunzaji mwingine wowote kutokana na kuiga modeli katika ingizo, kufanya mazoezi ya hiyo tabia mpya na kutoa mrejesho sahihi. Kwa mfano, mjifunzaji hujifunza jinsi watu wengine wanavyotamka sauti au maneno fulani, naye huiga na kufanya mazoezi ya utamkaji kutoka kwa wasemaji wazawa na hatimaye huweza kutamka kwa usahihi.

Aidha, kipengele kingine katika ujifunzaji kinaonesha kuwa mtu hujifunza bila kujua wakati mchakato wa kujifunza unapoendelea. Wanautabia hudai kuwa ujifunzaji hutokea nje ya ung'amuzi tambuzi; hakuna michakato ya akili inayohusika, bali vichocheo vya nje hutokana na mwingiliano na mazingira ya mjifunzaji. Hii inadhihirisha kwamba lugha ni aina ya utamaduni na mwanadamu hutumia lugha kama njia ya kuwasiliana.

Nadharia ya ujifunzaji ya utabia inatoa kielelezo kizuri hasa katika mchakato wa ujifunzaji lugha. Kwa mujibu wa Thorndike (1911), kuna viashiria viwili vya Nadharia ya Utabia katika ujifunzaji lugha, navyo ni vya kinadharia na kiutendaji. Katika kiashiria cha kinadharia, kiashiria cha utabia kimekitwa katika nadharia ya ujifunzaji katika utabia. Thorndike anaeleza kuwa sheria/kanuni nne za ujifunzaji zinatoa mchango mkubwa katika ujifunzaji lugha. Katika kiashiria cha kiutendaji, Thorndike anatilia msisitizo umuhimu wa desturi/mazoea na hatua za ujifunzaji, hasa mchakato wa ujifunzaji lugha (katika Barash, 2005).

Kwa mujibu wa Skinner (1976), viashiria vya kinadharia vya nadhariatete ya uzoeshi-fanyizi vinaunda lugha ya tabia fanisi, msamiati na sarufi; lugha hiyo ni lazima ihusu tukio la kitabia ili iweze kuelezwa kwa usahihi. Kati ya mambo muhimu ya lugha ya sasa katika nadhariatete fanyizi ni tofauti kati ya miitikio iliyoachwa na iliyoshawishi, upanuzi wa msamiati huu unagawa matumizi ya mwitikio. Lugha ya tabia inaweza kuwa fanisi zaidi katika upanuzi kwenye tabia ya maneno. Kuzungumza na kuandika ni aina za tabia, ila msamiati unaleta ugumu katika tabia hizo. Kwa mfano, mwanadamu anazungumza kwa kutumia maneno. Msamiati haushindwi tu kutofautisha tabia ya maneno yaliyoandikwa kwa yaliyozungumzwa, bali pia unayafanya maneno kama vitu badala ya aina ya miitikio. Mara kwa mara, tabia ya maneno inachukulia au inafanya kama Skinner alipata lugha zote kutoka kwenye uhusiano wa kichocheo-mwitikio kati ya aina nyingine za utabia (Gazda na Raymond, 1980).

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imefafanua jinsi Nadharia ya Utabia inavyoweza kutumika katika ufundishaji wa lugha ya kigeni kwa wajifunzaji wapya. Makala inajenga hoja kwamba tabia ya mwanadamu ni matokeo ya ujifunzaji. Hivyo, inaweza kubadilishwa kwa kutengeneza au kuunda masharti ya ujifunzaji. Makala hii inadhihirisha kuwa Nadharia ya Utabia inaweka msisitizo mkubwa kwenye kujenga tabia ili ionekane katika mazingira husika. Vilevile, nadharia hii inawekea mkazo kwenye nafasi ya mazingira katika ujifunzaji na ufundishaji, inajihusisha na uundaji wa athari au mwitikio, inasisitiza umuhimu wa mazoezi katika kujenga uzoeshi wa tabia iliyokusudiwa, inajihusisha na utaratibu wa utokeaji wa matokeo ya ujifunzaji pamoja na umuhimu wa uwezo na matokeo ya ujifunzaji yanayopatikana katika uzalishaji wa tabia iliyokusudiwa. Katika Nadharia ya Ujifunzaji, tabia ya mwanadamu inadhibitiwa na tuzo au adhabu ambayo ni kiimarisho chanya au hasi kutoka katika mazingira. Hivyo, tabia ya ujifunzaji inaingiliana sana na mwitikio wa

kitabia na kichocheo. Kwa hiyo, Nadharia ya Utabia haiwezi kuachwa kabisa kwa sababu kuna vipengele vingine vya msingi ambavyo ni muhimu sana katika ufundishaji kama vile kutoa mazoezi, kufundisha kwa kuzingatia mazingira na wakati mwingine mazoezi ya kurudiarudia inapobidi.

## Marejeleo


Alissa, D. (2003). Behaviourism: More than a failure to follow in Darwin's footneteps, *American History*, 87(2):686-700.

Barash, D.P. (2005). *B. F. Skinner Revisited: The Chronicle of Higher Education*. Washington: Vintage Books.

Blankship, (1981). *Mainstreaming Students with Learning and Behavior Problems: Techniques for the Classroom Teacher*. New York: Holt Rinehart and Winston.

Brown, H.D. (1994). *Teaching by Principles: An Interactive Approach to Language Pedagogy*. New Jersey: Prentice Hall Regents.

Fauziati, E. (2014). *Methods of Teaching English as a Foreign Language (TEFL): Traditional Method, Designer Methods, Communicative Approach, Scientific Approach*. Surakarta: Era Pustaka Utama.

Fauziati, E. (2016). *Applied Linguistics: Principles of Foreign Language Teaching, Learning, and Researching*. Surakarta: Era Pustaka Utama.

Gadza, M.G. and Raymond, J. (1980). *Theories of Learning Comparative Approaches*. Illinois: Peacock Publisher Inc.

Johnson, K. (2001). *An Introduction to Foreign Language Learning and Teaching*. Harlow: Pearson Education Limited.

Leahey, T.H. (2000). *A History of Behavioural Psychology*. New York: Freeman.

Lodico, M.G., Spaulding, D.T. and Voegtle, K.H. (2006). *Methods in Educational Research: From Theory to Practice*. San Fransisco: Jossey-Bass.

Sarah, E.I. (2006). Bending Behavior American Scientist. *Research Triangle Park*. 94(3):267-286.

Skinner, B.F. (1976). *About Behaviourism*. New York: Vintage Books.

Staats, W. and Staats, K. (1963). *Complex Human Behavior: A Systematic Extension of Learning Principles*. New York: Holt, Rinehart & Winston.

Staddon, J. (2014). *The New Behaviourism*, 3rd Edition. Philadelphia: Psychology Press.

Thorndike, E. L. (1911). *Animal intelligence: Experimental Studies*. New York: Macmillan.

Watson, J.B. (1913). Psychology as the Behaviourist views it, *Psychological Review*. 20:158-177.

Windholz, G. (1997). Ivan P. Pavlov: An Overview of his life and Psychological work. *American Psychologist*. 52(9):941-958.